



Muda: Saa 2

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina: _____

Shule: _____

Nambari ya Tathmini/UPI: _____

Tarehe: _____

Maelekezo kwa Wanafunzi

- Andika jina lako, Nambari yako ya Tathmini/UPI na tarehe katika nafasi ulizopewa.
- Kagua karatasi ya maswali kwa makini ili kuhakikisha kurasa zote zimechapishwa na hakuna swali lililoachwa.
- Jibu maswali yote katika nafasi ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SEHEMU	% YA ALAMA	Kuzidi Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Chini ya Matarajio	Maoni ya Mtahini
Kiwango cha Alama		75-100	40-74	21-39	1-20	
Alama za Mwanafunzi						
Kiwango		4	3	2	1	
Weka Alama ya ✓						

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

- Soma kifungu kifuatacho kisha uchague jibu sahihi la kujazia kila nafasi.

Watoto wengi wanaoishi mitaani ni maskini au mayatima. Hapo zamani, watoto wa aina **(1)** walikuwa wakitunzwa na ukoo **(2)**. Siku **(3)** mambo **(4)** katika miji mikubwa, ambapo watoto wengi wanazurura barabarani **(5)** chakula. Watu wengine **(6)** hata hawaangalii bali huendelea na shughuli zao. Wao hufikiri kuwa hakuna mtu **(7)** mwenye akili timamu **(8)** kuzurura bila sababu.

No.	A	B	C	D
1.	hiyo	hii	hao	hizi
2.	wao	yao	chao	wake
3.	hizi	hii	hao	hiyo
4.	limebadilika	yamebadilika	imebadilika	amebadilika
5.	akiomba	wakiomba	waliomba	wameomba
6.	wakiwaona	akiwaona	tukiwaona	mkiwaona
7.	wowote	yoyote	yeyote	wote
8.	ambaye	ambayo	ambao	ambamo

- Neno *kilema* liko katika ngeli gani?

A. KI-VI B. A-WA C. U-ZI D. LI-YA

- Kauli ya kutendana ya kitenzi *penda* ni ipi?

A. Pendeka B. Pendea
C. Pendana D. Pendapenda

- Mtu anayesafiri na kuendesha ndege huitwa nani?

A. Dereva B. Nahodha C. Rubani D. Fundi

- Kinyume cha neno *anika* ni kipi?

A. Anakia B. Funika
C. Andika D. Anua

13. Kifaa kinachotumiwa kupiga simu na kutuma ujumbe pia huitwa:

- A. Runinga B. Tarakilishi
C. Kipepesi D. Simu

14. Kamilisha tashbihi ifuatayo:

Mweusi kama _____.

- A. Giza B. Mkaa C. Maji D. Theluji

15. Baba ya baba yangu ni nani kwangu?

- A. Mjukuu B. Babu
C. Baba mkubwa D. Binamu

16. Kamilisha methali ifuatayo:

Mchumia juani hulia _____.

- A. nyumbani B. kivulini
C. shambani D. njiani

17. Kisawe cha neno *kijiji* ni kipi?

- A. Karia B. Jiji C. Mtaa D. Kisura

18. Kanusha sentensi hii: *Amelala*.

- A. Hajalala B. Hakulala C. Halali D. Hajalali

19. Mawingu mazito ya mvua mara nyingi huwa na rangi gani?

- A. Nyeupe B. Nyeusi C. Njano D. Nyekundu

20. Taja nomino ya pekee kutoka kwenye maneno yafuatayo.

- A. Mwalimu B. Msichana C. Nairobi D. Kitabu

21. Chagua sentensi iliyoandikwa kwa matumizi sahihi ya alama za uakifishaji.

- A. Maria Petro na Natalia.
B. Maria, Petro na Natalia.
C. Maria Petro, na Natalia.
D. Maria; Petro Natalia?

22. Kitanda maalumu kinachotumiwa kubeba wagonjwa hospitalini huitwa:

- A. Gurudumu B. Machela
C. Shubaka D. Kipamajoto

23. Matibabu anayopatiwa mgonjwa kabla ya kufikishwa hospitalini huitwa:

- A. Huduma ya kwanza
B. Kulazwa
C. Kupepetwa
D. Kupewa dawa

SEHEMU B: KUSOMA NA KUELEWA

17. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Amani ni mwanafunzi wa umri wa miaka kumi na moja. Anaishi katika kijiji cha Upendo na anasoma katika Shule ya Msingi ya Tumaini. Amani yuko katika Gredi ya Tano.

Amani ni mtoto mwenye afya njema na anayejitunza vizuri. Nywele zake huwa safi na kuchanwa kwa nadhifu. Kucha zake huwa fupi na safi. Wazazi na walimu wake humpongeza kwa kupenda usafi.

Wenzake wanampenda kwa sababu huwashauri kuwa na bidii, heshima na nidhamu. Anapoonza mwanafunzi akifanya kosa, humkosoa kwa upole na kumshauri abadili tabia. Amani huamini kuwa wanafunzi wanaposhirikiana na kupendana, hujenga urafiki na umoja shuleni.

Amani pia ni mwanachama wa klabu ya mazingira. Yeye pamoja na wenzake huwafundisha watu umuhimu wa kutunza mazingira. Hufagia uwanja, hufyeka nyasi na kutupa taka kwenye vyombo vinavyofaa.

Amani ni mfano mwema kwa jamii. Ana tabia ya kuwasalimia wakubwa na wadogo kwa adabu. Watu wengi wamejifunza tabia njema kutokana na mwenendo wake.

24. Kifungu ulichosoma kinamzungumzia nani?

A. Maria B. Mwalimu C. Amani D. Wazazi

25. Amani yuko katika Gredi ya:

A. Tatu B. Nne C. Tano D. Sita

26. Wenzake wanampenda Amani kwa sababu anawashauri kuwa na:

A. Utajiri B. Heshima C. Uvivu D. Hasira

27. Mwanafunzi anayekiuka nidhamu huwa na:

A. Tabia njema B. Tabia mbaya
C. Bidii nyingi D. Heshima kubwa

28. Njia mojawapo ya kutunza mazingira iliyotajwa kwenye kifungu ni:

A. Kuharibu mimea B. Kutupa taka ovyo
C. Kufyeka nyasi D. Kuchoma vitabu

29. Ni jambo gani linaonyesha kuwa Amani ni mfano mwema katika jamii?

A. Kuwatukana watu
B. Kuwasalimia watu kwa adabu
C. Kupigana na wenzake
D. Kukataa ushauri

30. Umejifunza nini kutokana na kifungu hiki?

A. Tabia njema B. Uvivu
C. Wivu D. Ubinafsi

31. Ni methali gani inayoendana vizuri na kifungu hiki?

A. Wema hauozi
B. Haraka haraka haina baraka
C. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
D. Mkataa pema pabaya panamuita

32. Amani ni mwanachama wa klabu gani?

A. Klabu ya michezo
B. Klabu ya muziki
C. Klabu ya mazingira
D. Klabu ya drama

33. Kichwa gani kinafaa zaidi kwa kifungu hiki?

A. Sokoni Kwetu
B. Amani, Mtoto Mwenye Tabia Njema
C. Safari ya Shuleni
D. Mvua Kubwa

SEHEMU C: SARUFI NA MSAMIATI

34. Tumia kiambishi sahihi kujazia nafasi.

Waraka huo _____likuwa mrefu.

A. a B. I C. u D. zi

35. Tumia kiambishi sahihi.

Nyavu _____naelea majini.

A. ki B. zi C. u D. a

36. Kamilisha tashbihi ifuatayo:

Mchoyo kama mkono wa _____.

A. baba B. birika C. mama D. mtoto

37. Kamilisha tashbihi ifuatayo:

Shujaa kama askari _____.

A. kanzu B. maji C. vitani D. darasani

38. Chagua sentensi yenye matumizi sahihi ya lugha.

A. Nimependa umoja wetu shuleni.
B. Mimi jana kuimba wimbo.
C. Wao mavazi ya kitamaduni jana.
D. Walishiriki ya maombi kitaifa.

Soma jedwali lifatalalo kwa makini kisha ujibu maswali nambari 1 na 2.

Siku	Shughuli ya Chebet	Shughuli ya Juma
Jumatatu	Kusafisha vyombo	Kuosha gari
Jumanne	Kusoma riwaya	Kucheza mpira
Jumatano	Kupanda mboga	Kupalilia bustani
Alhamisi	Kupika chakula	Kuteka maji
Ijumaa	Kusaidia maskini	Kupumzika

39. Baada ya kuchanganua shughuli za watoto hawa wiki nzima, ni hitimisho gani *sahihi kabisa* unaweza kufanya kuhusu tabia za Chebet na Juma?

- A. Juma ana bidii kuliko Chebet kwa sababu yeye huosha gari na kucheza mpira.
- B. Chebet anatilia maanani zaidi kazi za nyumbani na matendo ya uzalendo kuliko Juma.
- C. Chebet na Juma wote wanajali afya zao kwa sababu wanapenda kupumzika Ijumaa.
- D. Juma hapendi kufanya kazi za nyumbani kwa sababu yeye huteka maji tu.

40. Fikiria kuwa Jumatano ni siku ya utunzaji wa mazingira shuleni. Ni ushahidi gani kutoka kwenye jedwali unaothibitisha kuwa Chebet na Juma tayari wana ujuzi wa kutunza mazingira?

- A. Wote wawili wanapenda kufanya kazi za nyumbani siku ya Alhamisi.
- B. Juma huosha gari huku Chebet akisafisha vyombo siku ya Jumatatu.
- C. Chebet hupanda mboga naye Juma kupalilia bustani siku ya Jumatano.
- D. Chebet husaidia maskini naye Juma akipumzika siku ya Ijumaa.

MAJIBU

1. A
2. A
3. A
4. B
5. B
6. A
7. C
8. A
9. A
10. C
11. C
12. B
13. D
14. B
15. B
16. B
17. A
18. A
19. B
20. C
21. B
22. B
23. A
24. C
25. C
26. B
27. B
28. C
29. B
30. A
31. A
32. C
33. B
34. C
35. B
36. B
37. C
38. A
39. B
40. C